JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

636 **TEHAMA**

Muda: Saa 3 Hours **Mwaka: 2024**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa ufupi nyenzo nne anazotakiwa kuwa nazo mwalimu katika maandalizi ya mpango kazi wa somo la TEHAMA.
2. Fafanua namna ya kutumia mbinu ya ufundishaji unaochochea udadisi.
3. Eleza kwa kifupi mambo manne ya kuepuka katika ujifunzaji.
4. Bainisha kwa ufupi udhaifu wa maswali ya “kweli au si kweli” katika upimaji wa somo la TEHAMA.
5. Bainisha vigezo vya kuzingatia wakati wa kubuni na kufaragua zana.
6. Changanua kwa mfuatano nyanja nne za mwanzo za Benjamini Bloom ambazo hutumika katika utunzi wa mitihani na majaribio.
7. Eleza tabia walizonazo wanafunzi wanaojifunza kwa vitendo.
8. Eleza kwa kifupi namna ambavyo redio, luninga, vitabu na simu za mkononi vinavyoweza kutumika katika kufundisha mada ya “kueleza kwa usahihi habari iliyosemwa.”
9. Ainisha mambo yanayoweza kuchangia ufaulu wa mwanafunzi.
10. Fafanua kwa kifupi umuhimu wa mwelekeo unaohitaji utafutaji, uchambuzi na uwasilishaji wa habari na taarifa katika ujifunzaji wa somo la TEHAMA.

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia hoja tano eleza umuhimu wa kubuni na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA.
12. Eleza sababu za ufundishaji wa vitendo kuwa na tija zaidi kuliko ufundishaji wa nadharia pekee.
13. Kwa kutumia hoja tano fafanua madhara ya wanafunzi wanaosoma mafunzo ya Ualimu kutoshiriki ufundishaji kifani.
14. Ainisha zana tano zinazoweza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.